**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

Shule ya Sekondari Mafisa,
S. L. P. 24,
**SONGE - KILINDI.**

**SIMU: 0686767617/0625444299**
**0625 - 986182/0784 - 111668**

E-Mail:mafisasec24school@gmail.com

**Kumbu Na.MFS/JN/FV/01/03**

**MWANAFUNZI:**
**SHULE YA SEKONDARI………………………………………………………………**

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Kwa barua hii nakujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha Tano mwaka 2022/2023 shule ya Sekondari Mafisa katika mchepuo wa………………………………… unatakiwa kufika Shuleni kuanza masomo tarehe…………………………………………… na ufike kabla ya saa kumi na mbili (12.00) jioni. Siku na saa ya mwisho ya kuripoti ni tarehe ………………………….. saa…………….Shule hii ipo Mkoa wa Tanga katika Wilaya ya Kilindi, shule ipo Kijiji cha Mafisa kilometa 21 kutoka Makao makuu ya Wilaya Kilindi.

Kwa wanafunzi wanaotokea Dar es-salaam watapanda mabasi yanayoelekea Songe watafikishwa kwenye kijiji cha Mafisa mahali ilipo Shule hii, Kwa wale wanao tokea Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro watashuka kwenye Mji wa Handeni au Korogwe na Kupanda mabasi yanayoelekea Songe. Kwa wale wanaotokea Mikoa ya Nyanda za juu Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya kati watafika Dodoma na kupanda mabasi yanayopitia njia ya Gairo au Kiteto watafikishwa kwenye kijiji cha Mafisa ilipo shule hii. **TUNAWATAKIA SAFARI NJEMA**- **KARIBUNI SANA.**

Siku ya kuripoti mwanafunzi aje akiwa amevaa suluali ya kushindia (NYEUSI) na Tisheti ya Michezo (LIGHT BLUE) na viatu vya Darasani au Raba ya michezo.

Nguo zingine za nyumbani kama jinsi, Buti, Tshirt za nyumbani, Kofia na nyinginezo **HAZIRUHUSIWI SHULENI.**

Wanafunzi wote wapimwe afya zao na wajaziwe na walete fomu iliyoambatanishwa ikiwa na taarifa ya Daktari.

Mkuu wa shule, walimu wote na wafanyakazi wote wa shule hii wanakupongeza na wanatarajia uwe mwanafunzi **MTIIFU, NADHIFU, MWAMINIFU** na mshiriki mzuri wa kazi zote za nje na ndani ya darasa

Kwa mawasiliano piga namba **0686767617/0625 - 986182**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MAFISA**

................................
**CHARLES HARUNI MGOMBA**
**MKUU WA SHULE**

## 1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1.1 SARE ZA SHULE

i. Suruali 2 rangi ya kijivu yenye malinda mawili kila pande isiwe inabana kwa ajili ya sare ya darasani,suruali 2 rangi nyeusi kwa ajili ya shughuli za nje
ii. Shati 2 nyeupe yenye mikono mirefu lisiwe fupi na linalobana
iii. Sweta ya kijivu
iv. Viatu vyeusi vyenye kamba, visiwe vilivyochongoka na visiwe na shingo, kisigino kirefu, soksi pea mbili nyeusi
v. Mkanda mweusi usiwe na bakozi kubwa
vi. Fulana mbili rangi Light Blue
vii. Nguo za michezo - Track suit Dark blue na raba za michezo

### 1.2 MALAZI:

i. Shuka 2 - Light blue
ii. Mto na foronya zinazofanana na shuka
iii. Godoro upana futi 2.5 na unene inchi 4
iv. Chandarua na blanketi
v. Aje na nguo za kulalia

### 1.3 VYOMBO VYA CHAKULA

i. Sahani
ii. Kijiko
iii. Kikombe (Vyombo hivyo visiwe vya Plastiki)

### 1.4 VIFAA VINGINE

i. Ndoo kubwa 1 na ndogo 1
ii. Mswaki, Taulo, malapa na sabuni
iii. Madaftari makubwa saba (Counter book)
iv. Jembe na kwanja
v. Sanduku la bati na kufuli (TRUNKER)
vi. Aje na vitabu vya Mchepuo wake
vii. Aje na rimu ya karatasi nyeupe A4

### 1.5 MALIPO

| MAHITAJI | MUHULA WA 1 | MUHULA WA II | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Ada | 35,000 | 35,000 | 70,000/= |
| Taaluma | 15,000 | - | 15,000/= |
| **Huduma ya afya**<br>Asiye na kadi ya bima ya afya | 20,000 | - | 20,000/= |
| Mwenye kadi ya bima ya afya | 10,000 | - | 10,000/= |
| TAHADHARI | 5000 | - | 5000/= |
| UPISHI | 10,000 | 10,000 | 20,000/= |
| DAWATI | 20,000 | - | 20,000/= |
| FULANA 2 | 30,000 | - | 30,000/= |
| ULINZI | 10,000 | - | 10,000/= |
| UKARABATI | 10,000 | 10,000/= | 20,000/= |
| KITAMBULISHO | 5000 | - | 5,000/= |
| **JUMLA**<br>**Mwenye kadi ya bima ya afya** | **150,000** | **55,000/-** | **205,000/=** |
| **Asiye na kadi ya bima ya afya** | **160,000** | **55,000/=** | **215,000/=** |

Fedha za Ada zilipiwe NMB Benki Akaunti namba
**42601100026. JINA LA AKAUNTI -MAFISA SECONDARY SCHOOL CAPITATION.**
Mwanafunzi aje na nakala halisi ya Benki Slip ikiwa imeandikwa jina halisi la Mwanafunzi

- Kwa wanafunzi wanaogharamiwa na Serikali waje na uthibitisho toka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri anakotoka
- Wafadhili wengine walipe kabisa

**NB: NGUO ZA NYUMBANI PAMOJA NA SIMU HAVITARUHUSIWA KABISA SHULENI**

Mwanafunzi aje na

- Nakala moja ya CHETI CHA KUZALIWA
- Nakala ya RESULT SLIP
- Picha tatu (3) (PASSPORT SIZE) zenye BACKROUND BLUU apige akiwa na shati nyeupe

## 2.0 SHERIA ZA SHULE

2.1 Mwanafunzi atazingatia mambo yafuatayo:-

i. Kuhudhuria vipindi vyote vya darasani
ii. Kushiriki vizuri katika kazi
iii. Kuwahi katika kila shughuli
iv. Kusalimia walimu na walezi wote
v. Kuhudhuria mikutano yote shuleni
vi. Kutokwenda nje ya shule bila kibali maalumu
vii. Hairuhusiwi kutumia lugha mbaya Shuleni
viii. Kuvaa sare za shule muda wote na kuzingatia ratiba ya shule
ix. Kuitika na kukimbia anapoitwa

## 2.2 MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
v. Uvutaji bangi, tumbaku nk
vi. Kupiga au kupigana
vii. Kudharau Bendera ya Taifa na alama zingine za Taifa. mf, wimbo wa Taifa
viii. Kuoa
ix. Kusababisha mimba
x. Kugoma au kuchochea mgomo
xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
xii. Kuwa na simu ya mkononi
xiii. Kuja na heater/ kuwa na heater

***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MAFISA***

……………………………
**CHARLES HARUNI MGOMBA**
**MKUU WA SHULE**

# REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
# MAFISA SECONDARY SCHOOL
# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS

MAFISA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 24
**SONGE – KILINDI**

Date…………………

**MEDICAL OFFICER, GOVERNMENT HOSPITAL**
………………………………………………
NAME OF STUDENT…………………………………………
Please examine the above named student to ascertain his fitness for admission to pursue studies.

…………………………………………
**Headmaster**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin……………………………………………………………………………………………………
Eyes……………………………………………………………………………………………………
Ears……………………………………………………………………………………………………
Chest…………………………………………………………………………………………………
Spleen…………………………………………………………………………………………………
Abdomen………………………………………………………………………………………………
Urine……………………………………………………………………………………………………
Stool……………………………………………………………………………………………………
Hemoglobin (Hb)………………………………………………………………………………………
I consider that:

1. He is of good health, free from infectious diseases, worms, bilharzias and fit to pursue studies
2. He is now fit to return to school after having been treated for……………………….

………………………………… …………………………………
**Name and Designation** **Signature**

…………………………… ……………………………
**Official Stamp** **Date**

# UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MAFISA

**SEHEMU A:** (Ijazwe na Mwanafunzi)

Mimi (jina kamili)…………………………………………………………………………………

Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………………………

Dini……………………………………………………………………………………………

Kijiji…………………………… Wilaya………………………… Mkoa……………………………

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia Kidatocha Tano Shule ya Sekondari Mafisa. Nathibitisha kuwa Nitatii na kufuata sheria zote za Shule kama zilivyo ainishwa. Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiriki katika Migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa Shule ili matatizo yatafutiwe ufumbuzi pindi yanapotokea.

Saini………………………………………… Tarehe……………………………………

**SEHEMU B:** (Ijazwe na Mzazi)

Mimi (Jina kamili) ……………………………………………Namba ya simu……………………

KIjiji…………………………… Wilaya……………………… Mkoa…………………………

Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mwanangu Nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya Shule. Nitahakikisha mtoto anaenda shule muda uliopangwa na nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na Shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.

Saini ya Mzazi …………………………………………………Tarehe…………………………………

Jina la Mtendaji wa Kijiji………………………………………………………………………

Saini…………………………………… Tarehe………………………… Mhuri……………………

Jina la Mtendaji Kata……………………………………………………………………………

Saini…………………………………… Tarehe………………………… Mhuri……………………